

**Tumepitia hatua ndefu na ni wakati wa kubadilika.** Tumejivunia kuwa Kituo cha Wakimbizi cha Melaleuca. Hata hivyo, tumekomaa na kwa hivyo tunataka kitambulisho chetu kionyeshe kila jamii tunayo ihudumia na ahadi yetu ya uwajibu wetu wa kustahili.



**Tunauheshimu urithi wetu.** Alama yetu mpya inaonyesha uaminifu kwa ile ya zamani. Inaendelea kusimulia ile hadithi ya Melaleuca ikiwa ni mti unaowapatia kila mtu kivuli, una sifa za uponyaji na jina linalomaanisha ueusi na ueupe kwa uhalisi.



**Alama yetu mpya** inaangazia majani ya mti wa Melaleuca, kama chanzo cha maisha kwa mti huo pamoja na ubinadamu wote. Tunaonyesha maono yetu ya, Dunia ambayo kila mmoja anastahili, kupitia asili ya mviringo wa majani kwenye alama yetu, ikituonyesha dunia, jua na hata mwezi. Zaidi ya hayo yote, alama yetu inaonyesha uongozi.



**Jina letu ni Melaleuca Australia**** Wale watu tunaowakaribisha na kuwatumikia hawajafung-wa na kituo chochote. Wana uhuru wa kuchagua jinsi ya kuishi maisha yao katika jamii hii pana.



**Maadili yetu ndiyo msingi wetu.** Tumefanyiza upa Maono yetu, Dhamira na Maadili yetu ili yaangazie mtazamo wetu thabiti wa ubinadamu na utoaji huduma.

Tuko sasa

Melaleuca AUSTRALIA

Everyone belongs

*Jani jipya linalostawi ni kama maisha ya baadaye ya mti unao-ongoza njia.*

** Our legal name still remains as Melaleuca Refugee Centre – Torture and Trauma survivor services of the NT

# MAONO YETU

Dunia ambayo kila mtu anastahili

# DHAMIRA YETU

Tunaishi ili kuwakaribisha na kuwasaidia watu na familia zilizo na asili na tamaduni tofauti kuishi maisha yao jinsi watakavyo chagua.

# MAADILI YETU

**Kustahili** – Kuunda hisia ya ujamii ambapo kila mmoja anakaribishwa na anahisi kuwa anahusishwa

**Huruma** – kudumisha matendo ya huruma, upole na wema kwa kila mtu

**Maadili** – Kutekeleza majukumu yetu ya kiadilifu kwa kila mmoja wetu, watu tunaowatumikia pamoja na jamii.

**Heshima** – Kumkubali kila mmoja kama mtu wa kipekee.

**Wajibu** – Kuwajibika kwa kila kitu tunachokifanya na jinsi tunavyokifanya kutoka mwanzo hadi mwisho.

- Majani kuwa pamoja kama ishara ya umoja- wale tunaowatumikia na wale tunatumikiana nao.
- Jani jipya limechukua nafasi yake halali/ linapostahili.

- Picha ya kipamoja ya mwendo wetu sote tukielekea katika mafanikio.
- Jani jipya linalostawi – maisha yetu machanga ya baadaye yakiongoza mwendo.




- Upendo wa moyo iliyowekwa katikati ya alama yetu.
- Muungano wa majani unaochukua umbo la parafujo, umeunganishwa katika uhusiano.

- Jani la Melaleuca linaashiria uponyaji.
- Majani yanaashiria usanisinuru na maisha.

Melaleuca
AUSTRALIA
Everyone belongs